

## TANGAZO KWA UMMA

Shukrani kwa nia yako ya kutaka kushiriki katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP una sera ya ajira iliyowazi na inayoelekeza kuwa fursa ya ajira inatakiwa kutangazwa katika magazeti nchini Tanzania na Uganda na kuwekwa katika ukurasa wa tovuti ya Mradi wa EACOP.

Tangazo lolote la ajira linalotangazwa bila kuzingatia hatua hizi linatakiwa kutiliwa mashaka na kutambulika kuwa haliusiki na Mradi. Ukiona tangazo lolote la kazi za Mradi wa EACOP linalotia mashaka tafadhali toa taarifa katika kituo chochote cha polisi karibu yako, Mamlaka ya Serikali za Mtaa au katika Mradi wa EACOP.

Maombi yote ya fursa yanatakiwa kuwasilishwa kwa Mradi kupitia njia zilizotangazwa. Maombi yatakayo wasilishwa kwa njia zisizo rasmi hayatozingatiwa.

Mradi una mchakato wa wazi wa kutoa fursa za ajira na unaozingatia ushindani. Washindani wanachaguliwa kwa kuzingatia vigezo na kwa kuzingatia sheria za ajira za nchi husika nchini Tanzania na Uganda.

Fursa za mafunzo kwa vitendo zinatangazwa katika ukurasa wa tovuti ya Mradi wa EACOP wenye matangazo ya ajira.

Unashauriwa kuendelea kutembelea ukurasa wa tovuti ya Mradi wa EACOP ili kuweza kupata taarifa za fursa za ajira kwa wakati.

- **Mwisho**-

**Kwa taarifa zaidi au kufanya mahojiano kwa ajili ya vyombo vya habari tafadhali wasiliana nasi kupitia:**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,  
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki – Tanzania / Uganda  
Mariagoreth Charles / Stella AMONY

**Simu ya ofisi:** +255 22 2214100/4102/4103 au +256 (0) 204 916 157

**Simu ya mkononi:** +255 699 000 341 au +256 794 888 157

**Baruapepe :** [mariagoreth.muangirwa@external.total.com](mailto:mariagoreth.muangirwa@external.total.com) au [stella.amony@external.total.com](mailto:stella.amony@external.total.com)

**Tovuti:** [www.eacop.co.tz](http://www.eacop.co.tz) au [www.eacop.com](http://www.eacop.com)